

**Mapatano mapya  
(1999) ya shirika ya  
kimataifa la wafanyikazi  
(SKW / ILO) juu ya  
aina mbaya zaidi za  
Ajira ya Watoto**



© ILO/IPEC Kenya



© ILO/IPEC Kenya

**Je wajua...**

© ILO/IPEC Kenya

Kimeandikwa na:

kikundi cha mashirika yasiokuwa ya  
kiserikari cha Geneva kinachohusika na  
mapatano juu ya haki ya watoto.

**Kisehemu kinachohusika  
na Ajira ya Watoto.**



# **...kuhusu mapatano mapya ya shirika la kimataifa la wafanyakazi juu ya aina mbaya zaidi za ajira ya watoto?**

Mwandishi na Mhariri: Pins Brown  
Usanifu na Mpangilio: Becky Smaga  
Tafsiri (Kifaransa): Marguerite Harrison  
Tafsiri (Kihispania): Jorge Castilla  
Tafsiri (Kiswahili): Bobby Mkangi

Tifsiri ya Kiswahili imewezeshwa na:  
African Network for the Prevention and Protection  
Against Child Abuse and Neglect (ANPPCAN)  
Regional Office, Nairobi, Kenya

	YALIYOMO	UKURASA
<b>Kikundi kidogo cha Ajira ya Watoto cha Kundi la Mashirika</b>	1. Utangulizi	4
<b>Yasiyo Ya Kiserikali la Mkataba wa Haki Za Watoto</b>	2. Mapatano ya 182: sehemu kuu Na maana yake	5
<b>Kijitabu cha Kikundi kidogo cha Ajira ya watoto Kuhusu Mkataba wa 182.</b>	3. Pendekazo la 190: vipengele Muhimu na maana yavyo	7
	4. Mipango ya utendaji ya Ngazi za Kitaifa	10
	Ni nani anayeweza kufaidika Na mikataba hii	11
<b>“ Kutekeleza Sera za Ajira ya Watoto, Serikali ni lazima zitegemee sana uhamasishaji na ujihusishaji wa dhati wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali...changamoto Kwa Serikali ni kuunda na kuendeleza miungano dhidi ya Ajira za watoto zinazohusisha vikundi visivyo vya kiserikali na mara nyingine vya kujitolea vilivyo vya mashinani, sekta binafsi na watu binafsi.</b>	Mapatano ya 182 yanahusiana Vipi na Mapatano ya Haki Za watoto ya Umoja Wa Mataifa?	12
	Jukumu la SKW (ILO) Katika utekelezaji wa Mkataba wa 182 na Pendekazo la 190	13
	Jinsi Mashirika Yasiyo Ya kiserikali yanavyoweza Kutumia Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190 – Kujihusisha na mipango ya utendaji	14
<b>Kutekeleza Mkataba wa Haki za Watoto: Uhamasishaji wa rasilmali katika mataifa yenye mapato madogo.</b>	5. Togo: Uchunguzi kifani	15
<b>Ed. James R. Himes, 1995.</b>	6. Shirika la Undugu la Kenya	16
	7. Shirika la ustawi wa watoto la kenya	21
	8. Kituo cha Sinaga cha wanawake na ajira ya watoto	22
	9. Jukumu la muungano mkuu wa wafanyakazi (Cotu-K)	23
	10. Halmashauri Ya Tanzania Ya Maendeleo Ya Kijamii (Tacosode)	24
	11. Juhudi Za Shirika La Amwik Kuinua Ufahamu	27
	12. Machapisho yanayohusika Na Mapatano ya 182 Orodha ya machapisho na mahali pa kuyapata	28
	13. Mashirika yanayohusika na Anwani	29

‘ ’

# 1. Utangulizi

Kijitabu hiki Kimechapishwa na Kikundi kidogo kinachohusika na Ajira ya Watoto cha Kundi la Mashirika yasiyo ya Kiserikali la mapatano ya Haki za watoto. Kundi hili ni muungano wa zaidi ya Mashirika hamsini (50) ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali yaliyoko Geneva, ambayo azma yao ni kurahisisha uimarishajji, utekelezaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapatano ya Haki za watoto. Kundi hili limegawanyika kwa baadhi ya makundi madogo yanayogusia masuala ya viini mbali mbali. Moja ya hivyo ni hili la Ajira ya Watoto. Lina mashirika zaidi ya ishirini (20) ya kimataifa na ya kitaalamu.

Mapatano ya Haki za watoto ya Umoja wa Mataifa yaliopitishwa mwaka wa 1989, yalivutia usikivu na uangalifu wa Jumuiya ya kimataifa, maeneo na katika mataifa, kwamba masuala ya watoto ni haki za kibinadamu. Uzinduzi wa msingi wa mtazamo wa Haki za kibinadamu kwa watoto kuitia mapatano haya, ulikuwa ni kiini cha Mkataba wa 182 wa Shirika La Kimataifa La Ajira (ILO) wa 1999 kuhusu Mifumo mibaya zaidi ya Ajira ya Watoto unaozifuata nyayo za Mkataba wa Haki za Watoto ambao unapendekeza ulinzi wa watoto dhidi ya kazi zinazowadhuru na kuwanyonya.

**Kwa vikundi vya haki za watoto, dhamira ya kijitabu hiki ni kuonyesha uwezo uliopo katika kujihusisha na utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Watoto. Uchunguzi kifani unaonyesha jinsi uhamasishaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali unaweza kuondoa Mifumo mibaya zaidi ya ajira ya watoto.**

**Kwa mashirika yanayohusika na masuala ya Haki za Kibinadamu kwa upana zaidi na yale ambayo kazi yao inashughulikia**

ajira ya watoto, tunadhamiria kutoa utangulizi kwa Mkataba wa 182 na umuhimu wake kwa makundi na mashirika mbali mbali ya kitaalamu na ya mashinani.

## Shukrani...

Kikundi kidogo kuhusu ajira ya watoto cha Kundi la Mashirika yasiyo ya KiSerikali (NGO) kingependa kuwashukuru **ILO/IPEC na Azina ya Mradi wa Haki za Binadamu ya Afisi ya Masuala ya Kigeni na Jumuiya ya Madola ya Uingereza** kwa kugharamia mradi huu.

Shukrani kwa wafuatao waliota maoni yao:

World Vision International

Sehemu ya mawasiliano ya Fungamano la Mashirika yasiyo ya Kiserikali. "NGO Group Liaison Unit".

Muungano wa ulimwengu wa Mashirika ya Wanawake wa Kikatoliki-(World Union of Catholic Women's Organisations)  
Shirika la Kimataifa la Kutoa Utetezi wa Kisheria kwa watoto (Defence for Children International)

Save the Children Sweden;

Defence for Children International; Costa Rica,

International Federation – Terres des Hommes;

ILO/IPEC;

**-The NGO Group Focal Point on Sexual Exploitation of Children**

**-WAO – Afrique**

**- Shirika la Kimataifa linalopinga Utumwa (Anti-Slavery International)**

ILO inakadiria kwamba idadi ya watoto kama milioni 250 walio na umri kati ya miaka 5 hadi 14 wanaofanya kazi ulimwenguni, milioni 120 miongoni mwa wako katika ajira wakati wote. Milioni 80 wanakadiria kufanya kazi za aina mbaya zaidi. Idadi kubwa ya hawa watoto wanafanya kazi katika sekta ya kilimo na mwajiri mkubwa zaidi wa watoto wa kike ni sekta ya ajira ya nyumbani (kindani). 70% ya watoto walioajiriwa hufanya kazi zisizo na malipo za familia zao, ziwe nyumbani ama katika biashara ndogo ndogo, mahambani ama mijini.



## **2. Mapatano ya 182 (M182)**

**Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190 ni nyaraka zinazohusika na uharamishaji wa mifumo mibaya zaidi ya ajira ya watoto. kwa kutumia hatua za dharura za ubatilishaji.**

Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi (ILO) ni wakala wa kitaalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) uliowajibishwa kutunga na kutekeleza kanuni za kimataifa za ajira. ILO ndiyo wakala ya UN inayoshirikisha sio serikali peke zao, bali na washirikishi wa mashirika ya waajiri na ya waajiriwa kutoka kila nchi. Makao makuu yako Geneva, Switzerland (Uswizi); Juni 1999, kikao kikuu cha Kila mwaka cha ILO, na wajumbe waliowakilisha sekta tatu zilizotajwa mbeleni, walikubaliana kupitisha Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190. Toleo la Kirefu la yaliyomo katika nyaraka hizi, yamo katika kijitabu hiki. Mikataba hii pia inaweza kupatikana kupitia afisi za ILO ama katika afisi za maeneo – tazama ukurasa wa 23 kwa maeleo zaidi ama tazama katika mtandao wa ILO ambao anwani yake ni [www.ilo.org](http://www.ilo.org). Maeleo zaidi kuhusu ILO yamo katika sehemu ya 4 ya kijitabu hiki.

Dhamira kuu ya Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190 ni upigaji marufuku wa aina mbaya zaidi za ajira ya watoto. Hati hizi mbili zinasisitiza hatua za dharura zifaazo za kuondoa unyonyaji mbaya zaidi wa watoto na hatua zote ziwe zinazingatia muda – zinapaswa kuanzishwa punde serikali inapoidhinisha rasmi Mikataba hii. (Uidhinishaji rasmi wa mkataba uhusisha serikali kukubali kirasmi kufuata na kujalidiwa na kanuni za

kimataifa na kuwajibika palipo na shutuma za ukiukaji). Ambapo Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190, zinatambua kwamba, kinachosababisha watoto kuajiriwa hakiwezi kuondolewa mara moja, inapendekaze kuwa ni lazima hatua za dharura zichukuliwe. Pamoja, Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190 pia zinatambua kuwa utatuzi wa janga hili la ajira ya watoto utakuwa wa utaratibu na punde mifumo yote mibaya zaidi imeondolewa , mingine itachomozwa na kushughulikiwa. Mambo tofauti yanahusika yakijumuisha umaskini, ubaguzi na nafasi finyu za elimu.

Uungaji mkono wa kimataifa wa Mapatano ya 182 umekuwa mzuri zaidi na kwa sasa ndio mkataba uloidhinishwa rasmi na mataifa kwa upesi zaidi katika historia ya ILO. Mataifa 41 yalikuwa yamekwisha idhinisha rasmi mkataba huu kufikia mwisho wa Oktoba 2000 – orodha ya hivi sasa ya mataifa yaliyoidhinisha rasmi mkataba huu, inaweza kupatikana katika mtandao wa ILO. Mkataba wa 182 ulipata uwezo wa kisheria na kuanza kutumika Novemba 19, 2000. Ibara zote za mapatano haya zinayalazimisha mataifa yote yanayouidhinisha, baada ya mwaka mmoja tangu uidhinishaji. Pendekazo la 190 haliyalazimishi mataifa. Umuhimu wake ni kupendekaze na kurahisisha utekelezaji wa Mkataba wa 182.

## **Elementi Kuu Za Mapatano**

Masharti makuu ya Mapatano ya 182 ni ya kufafanua kiwazi ni hali zipi zinaweza kuchukuliwa kuwa mifumo mibaya zaidi ya ajira ya watoto, na kutaja mambo yote ambayo serikali zinapaswa kufanya kuona kwamba ajira za aina hii zimepigwa marufuku na kuondolewa. Mambo ya kutiliwa maanani katika Mapatano ya 182 ni:

## Fasiri

- ❖ Mtoto ni yejote aliye na umri chini ya miaka 18, pasi na vikwazo (ibara 2).

**Fasiri ya mifumo mibaya zaidi ya ajira ya watoto inajumuisha:**

- (a) Aina zote za utumwa ama vitendo vinavyofuanana na utumwa, kama vile utumwa kwa madhumuni ya malipo ya deni, uuzaji na uandikishaji wa watoto na kuwatumia katika mapigano kwa lazima.
  - (b) kuwatumia watoto katika ukahaba na ponografia.
  - (c) kuwatumia watoto katika mambo haramu kama vile utengenezaji, usafirishaji, na uuzaji wa madawa ya kulevya.
  - (d) Kazi zozote zinazoweza kudhuru afya, usalama na maadili ya watoto. (ibara ya 3).
- ❖ Lazima Serikali zipate ushauri wa mashirika ya waajiriwa kwa mwenendo rasmi ndipo kuafikiana kuhusu ajira zipi zinaweza kuchukuliwa kama kazi za hatari zaidi kulingana na Ibara ya 3(d), katika nchi zao. Ni lazima zitilie maanani kanuni za kimataifa kama Pendekazo la 190, na kwa utaratibu kuangalia na kupitia tena aina zote za ajira zinazojitokeza katika ufasiri wa kitaifa na kushauriana na mashirika ya waajiri na ya waajiriwa (ibara ya 4).

## Utekelezaji


**Serikali ziji funge zenewe katika:**

- ❖ Uteuzi wa bodi mwafaka ya kutekeleza miradi ya kitaifa ya kupigana dhidi ya uajiri wa watoto katika mifumo mibaya zaidi ya ajira. (Ibara 7)
- ❖ Kuyahuisha mashirika ya waajiri na ya waajiriwa katika usanifu na utekelezaji wa mipango hiyo (Ibara ya 6).
- ❖ Kuyapokea na kuyazingatia maoni ya vikundi vinavyohusika, (mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo katika kazi zao, hupambana na mifumo mibaya zaidi ya ajira ya watoto, watoto na vijana pamoja na familia zao, walioathiriwa na mifumo hii mibaya zaidi ya ajira) katika usanifu na utekelezaji wa miradi hii.
- ❖ Pokea ushauri wa mashirika ya waajiri na ya waajiriwa, yanapozindua ama kuteua harakati (mpango ama asasi) za kusimama utekelezaji wa mapatano ya 182 (Ibara 5).
- ❖ Tekeleza masharti ya mkataba yanayohakikisha adhabu mwafaka – kushtakiwa mahakamani ama adhabu za uhalifu (Ibara 7).

## **Kushughulikia kuhusika kwa watoto katika ajira ambapo wananyonywa**

Serikali zinapaswa kujifunga katika Harakati zinazozingatia muda:

- ❖ **Kuzuia uhusishaji wa watoto katika ajira zinazowadhuru.**
- ❖ **Kutambua umuhimu wa elimu katika harakati za kuondoa ajira ya watoto.**
- ❖ **Kutoa usaidizi ili kuwaondoa watoto kutoka hali za majanga.**
- ❖ **Kuchukua hatua za kuwakarabati na kuwaunganisha watoto upya na jamii baada ya kutolewa ajirani**
- ❖ **Kuwapa watoto nafasi ya kupata elimu ya kimsingi ya bure na palipo haja na uwezo, mafunzo ya kazi baada ya kuokolewa kutoka ajira hizi.**



© Glen Films, USA

## **3. Pendelekezo La 190- (P 190)**

Pendelekezo la 190 ni kama mwongozo wa Mipango Ya Kitaifa.

Inaupa upanuzi Mkataba wa 182 na kutambulisha vipengele ambavyo Serikali zinapaswa kuzingatia katika utekelezaji wa Mkataba huu. Mambo ya kutiliwa maanani ni:

### **Mipango ya Kitaifa ya Utendaji.**

**Mipango ya Kitaifa ya utendaji ndiyo mifumo ya utekelezaji wa Mapatano ya 182. Pendelekezo la 190-linazitambua taratibu mwafaka za utekelezaji, mionganini mwazo, uwezo uliopo katika uhusishaji wa jamii kwa jumla.**

**Unapendekeza serikali zizingatie maoni ya waajiri, waajiriwa, na taasisi za kiserikali zinazohusika na wengine wanaojihusisha na mifumo mibaya ya ajira ya watoto. Hawa ni kama: watoto na vijana wenyewe, familia zao na makundi mengine ambayo kazi zao zinadhihirisha kujifunga kwao na dhamira za Mkataba wa 182 na Pendelekezo la 190 kama ilivyoamuliwa na Serikali.**

Mipango hii ina wajibu wa:


- ❖ **Kudhihirisha kiwazi ni vitendo vipi vinachukuliwa kama mifumo mibaya zaidi ya ajira ya watoto**
- ❖ **Kuhakikisha kwamba vitendo hivi vinalaaniwa kiwazi kama vitendo vibaya zaidi vya unyonyaji**

- ❖ **Kuwazuia watoto kuingia katika ajira hizi**
- ❖ **Kuwatoa watoto kutoka ajira hizi**
- ❖ **Kuwalinda watoto dhidi ya adhabu ama ukatili wowote unaoweza kutokana na kuwacha kazi**
- ❖ **Kuwapa watoto ukarabati na uunganishaji upya na jamii, unaozingatia mahitaji yake ya elimu, kimwili na kihisia**
- ❖ **Kuwa na uangalifu kuhusiana na watoto walio katika udhaifu zaidi: watoto wachanga: wasichana; na watoto wanaofanya kazi katika hali za kufichwa**
- ❖ **Utaratibu muafaka wa kupata, kufikia na kufanya kazi na jamii zilizo katika hatari zaidi.**
- ❖ **Kusambaza habari na uhamasishaji na kuongezea motisha ya utendaji katika jamii yote.**
- ❖ **Kufanya kazi katika mazingira yanayodhuru afya na kwa kutumia vitu vinavyodhuru**
- ❖ **Kufanya kazi katika hali za ugumu kwa masaa marefu, usiku ama kufungiwa katika mahali pa kazi (kwa mfano watoto wanaofanya kazi manyumbani na kuishi mle mle).**
- ❖ **Kazi iliyo na hatari inaweza kufanywa kihalali na watoto walio na umri zaidi ya miaka kumi na sita (16) lakini wawe wamelindwa dhidi ya janga lolote linaloweza kutokea kutokana na ile kazi, na kupata mafunzo ya kazi ile. Idhini ya kuruhusu kazi hizi ni lazima iafikiwe kupitia makubaliano na mashauriano baina ya mashirika/ makundi ya waajiriwa na ya waajiri.**

## **Kazi Ya Hatari.**

Mifano dhahiri ya kinachomaanishwa katika ibara ya 3 (d) ya Mkataba, ambapo kazi zile watoto wanazozifanya, zinawatumbukiza katika hatari ambazo hawawezi kuziepuka:

- ❖ **Kazi ambazo zinawafanya watoto kunyanyaswa kimwili, kisaikolojia na kimaadili**



© Glen Films, USA

## **Utekelezaji.**

- ❖ Serikali ni lazima zitambue umuhimu wa habari na tarakimu za ajira ya watoto
- ❖ Habari na maelezo yakusanywe kuhusu wale wanaozikiuka harakati za kitaifa za kuangamiza mifumo mibaya zaidi ya ajira, ambapo serikali zina wajibika kufahamisha ILO mara kwa mara
- ❖ Ijapokuwa jukumu la kutekeleza Mkataba wa 182 limegawanywa baina ya mamlaka tofauti; mamlaka haya yanaserutishwa kutia bidii ili yafanye kazi pamoja na kwa mwelekeo mmoja.
- ❖ Pendekazo la taratibu muafaka za kusaidia utekelezaji wa 182 na Pendekazo la 190 (kwa maelezo zaidi, tazama sehemu kuhusu wajibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na makundi mengine).

## **Adhabu.**

- ❖ Inapendekewa kuwa aina zote za ajira ya watoto katika ibara za 3(a) (b) na (c) za Mkataba wa 182 zifanywe ziwe makosa ya jinai
- ❖ Adhabu, zikijumuisha adhabu za kijinai inapohitajika, zitumiwe wakati mipango ya kitaifa ya kuondoa na kupiga marufuku ajira zinazodhuru, (zilizofafanuliwa katika ibara ya 3 (d) ya Mkataba) zinapokiukwa.
- ❖ Nchi tofauti zinapaswa kushirikiana katika ngazi ya kimataifa nyakati ajira hizi zinahusisha makosa ya kijinai ya

kimataifa na kuona kwamba watu wanaotenda makosa haya wanasa jiliwa

- ❖ Serikali ni lazima ziamue ni nani anayewajibika wakati sheria za kuzuia ajira mbaya zaidi ya watoto, zinapokiukwa.
- ❖ Serikali zinapaswa kutunga masuluuhisho ya kisheria na ya njia nyingine ya kutekeleza miradi ya kitaifa, kama inavyofaa.

## **Ushirikiano na Usaidizi.**

- ❖ Wanachama au wahusika wanapaswa kushirikiana na kusaidiana ili kutekeleza Mkataba, wakijumuisha msaada ulioimarishwa katika ustawi wa jamii na uchumi, uondoaji wa umaskini na elimu kwa wote.



## **4. Mipango ya Kitaifa ya Utendaji Ya Ngazi Za Juu - Wajibu wa mashirika ya Jamii.**

Katika sehemu hii, tutatazama fursa ambazo Mapatano ya 182 na Pendekero la 190 inazindua kwa Mashirika Ya Jamii, za kujihusisha katika mipango ya kitaifa ya utendaji iliyochapishwa kwa urefu katika kurasa za 12-21. (Kwa muktadha huu, mashirika haya ni yale yasiyohusishwa au kuwakilishwa rasmi na Serikali ama mashirika ya waajiriwa na waajiri yasiyo rasmi, na kwa hivyo kukosa kuwakilishwa katika ILO-tazama "Ni nani anayeweza kunufaishwa na hati hizi", chini).

Mashirika yamehusishwa katika uendelezaji wa Mapatano ya 182 na Pendekero la 190 kuanzia mbeleni. Uhamasishaji mkubwa zaidi ulikuwa unafanya kuhusu ajira ya watoto na ushirikiano baina ya mabara kuanzishwa, kufikia kuwasili kwa – "Matembezi ya Dunia ya Ajira ya Watoto" katika Jiji la Geneva mwezi wa Juni, 1998.

Mchango wa NGOs katika uandishi wa Mkataba wa 182 na Pendekero la 190 na athari yao nyakati za mwisho za uandishi katika Mkutano wa Kimataifa wa Ajira wa ILO wa 1999 ulikuwa na faida kubwa kwa toleo la mwisho, kudhihirisha umuhimu wa mchango kutoka sekta hii.

Ushurikiano kwa sasa unatoa msingi wa kisheria wa kupambana na ongezeko la uajiri wa watoto na kuyafunga mataifa kuchukua hatua muafaka. Jukumu la

mashirika haya katika mapambano dhidi ya ajira ya watoto limeelezwa katika ibara ya 6 ya Mapatano ya 182 na kufafanuliwa kwa urefu katika aya 2 ya Pendekero la 190, inayonakili kwamba mashirika yaliyojitokeza na kujifunga na utekelezaji wa maazimio ya mikataba hii, ni lazima, panapohitajika, kuona maoni yao yanazingatiwa katika usanifu na utekelezaji wa Mipango ya kitaifa. Hii ni nafasi kubwa kwa mashirika. Ni dhahiri kwamba wakati wa makabiliano, ni mashirika na makundi haya yaliyomo tu, katika nyakati fulani za ajira za watoto, kwa mfano; wakati kuna ajira ya watoto ya utumwa ama ukahaba na kwa hivyo ni mwafaka kwa miradi ya kuzuia, utendaji na mageuzi.

### **Ni nani anaweza kunufaishwa na hati hizi?**

Mashirika na makundi ya kitaalamu, yatapata kwamba Mapatano ya 182 na Pendekero la 190 yanaffaa kwa shughuli zao. Hati hizi zinaweza kutumiwa na:

- ❖ **Mashirika ya kimataifa na ya mashinani yasiyo ya kiserikali ya ajira ya watoto**
- ❖ **Makundi na miungano ya haki za watoto**
- ❖ **Mashirika yanayoshughulika na haki za kibinadamu na maendeleo**
- ❖ **Mashirika mengine ya kijamii yakijumuisha yale ya makundi ya jamii, ya wanawake na ya kidini**
- ❖ **Mashirika ya waajiriwa ambayo hayajawakilishwa kirasmi na ILO**

- ❖ **Makundi ya vijana, mashirika ambayo yanawakilisha watoto ama yanawahusisha watoto**
- ❖ **Makundi ya kitaalamu ya afya, elimu na sheria.**


## **Mapatano ya 182 yanahusiana vipi na Mapatano ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watoto (UNCRC)?**

Mapatano ya 182 na Pendekazo la 190 yanaupa nguvu ujumbe ambao UNCRC ilisisitiza wazi, kwamba watoto wana haki kama watu wazima na wanahitaji taratibu za kipekee ili haki hizo ziheshimiwe. Ibara ya 32 ya CRC inasema kwa kusisitiza “ kila mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya unyonyaji wa kiuchumi na kufanya kazi yoyote ambayo inaweza kutatiza elimu, ama kuwa na madhara kwa afya na ustawi wake, ama kuwa na madhara kwa afya au maendeleo ya kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na kijamii. Ujumbe huo huo umedhihirishwa wazi katika Mkataba wa ILO wa 138 wa 1973 kuhusu Umri Mdogo Zaidi Wa Kuingia katika Ajira. (Mkataba wa 182 haupitii tena ama kubatilisha Mkataba wa 138, ambao ni Mkataba mwingine wa kimsingi na umuhimu wa ILO wa kupiga marufuku ajira ya watoto kwa jumla).

Maarifa yanaweza kupatikana hapa kutokana na utekelezaji wa CRC. CRC ni mkataba uliofaulu zaidi katika upande wa uidhinashaji rasmi na kuungwa mkono kwa wingi na umma. Utaratibu wa utekelezaji wa CRC umeleta mtazamo wa kitaifa, kimaeneo na kimataifa wa masuala ya watoto na umezindua miungano mipana ya makundi ambayo kimsingi huwa na azma za haki na masilahi ya watoto yanayohusiana.

Matokeo yake ni kwamba, mashirika katika nchi nyingi yamefaulu katika ushawishi wa marekebisho ya sheria na sera zinazolinda haki za watoto na masuala yanayohusika.

Kwa kumalizia, mashirika haya yamechangia pakubwa katika uinuaji wa ufahamu wa umma kuhusu haki za watoto, kwa mfano afya, elimu na ushirikishwaji. (Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Miungano ya Kitaifa ya Haki za Watoto, tazama sehemu ya 8). Katika nchi nyingi, Mipango ya kitaifa ya kutekeleza CRC iko karibu, wazi na huchukua mwelekeo wa kushirikisha unaoleta pamoja sekta nyingi tofauti. Mipango hii inaonyesha kuchangia pakubwa katika kuzitia Serikali moyo, ili zifunge kwa Muda mrefu. Mafanikio ya miungano ya Haki za watoto (miungano ya mashirika yaliyojitelea kupigania haki za watoto) yanaonyesha kwamba taratibu zinazohusisha sekta nyingi ndizo zinazofaa; kwamba makundi yaliyo na maazimio yanayogongana yanaweza kuletwa pamoja na kuzindua masuluhihi yanayoweza kufaulu na kuwa shinikizo kwa Serikali na wengine, jambo ambalo linapaswa kudumishwa hata baada ya serikali kuidhinisha rasmi mkataba. Mashirika haya pia yamo katika nafasi nzuri ya kuhamasisha umma na kuzalisha mabadiliko katika mitazamo inayohitajika katika mageuzi. Miungano iliyomo ya mashirika ya haki za watoto iko katika nafasi nzuri ya kuzitia serikali na wengine moyo katika utekelezaji wa Mkataba wa 182.



© Glen Films, USA

## Jukumu la ILO katika utekelezaji wa Mkataba wa 182 na Pendelezo la 190.

ILO ni shirika muhimu katika utekelezaji wa mikataba hii. Ambapo muundo wa ILO unatambua rasmi mashirika ya waajiri, ya waajiriwa na Serikali. Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali yamedhihirisha wazi kuwa kuna fursa ya mashirika ya jamii kushirikiana pamoja na kushawishi pamoja na wanachama wa ILO. ILO ina miradi ya masuala ya kimatendo ya kupambana na ajira ya watoto- Mpango wa Kimataifa wa Kuondoa Ajira ya Watoto (IPEC), uliomo katika baadhi ya Mataifa.

Ushirikiano huanza na makubaliano baina ya Serikali na IPEC kuhusu jinsi watakavyofanya kazi pamoja. Hatimaye, IPEC hufanya kazi na Serikali, ikizisaidia kuanzisha Mipango ya Kitaifa ya Utendaji muafaka, ya kupambana na ajira ya watoto. Huendeleza miradi ya ngazi za mashinani na za Kitaifa likishirikiana na wahusika- Serikali na mashirika ya waajiri na ya waajiriwa – lakini pia kwa njia nyingi, mashirika ya kiraia.

**MATEMBEZI YA ULIMWENGU DHIDI YA AJIRA YA WATOTO (“GLOBAL MARCH AGAINST CHILD LABOUR”)**  
yanadhihirihisha jinsi watoto, vyama vya wafanyakazi, waajiri, mashirika yaliyo na mtazamo wa watoto na makundi mengine ya tabaka mbali mbali, yanaweza kuungana kwa azma moja ya kuondoa ajira mbaya zaidi ya watoto.

**Uzito wa uhusishaji wa vyama vya wafanyakazi katika nyanja za Kitaifa na za kimataifa, ulikuwa na ungali wa umuhimu katika kampeni hii.**

**Ushirikiano na vyama vya wafanyakazi ulikuwa wa umuhimu katika harakati za ushawishi wakati wa uandishi wa mswadajaribio wa Mkataba wa 182.**

**Ushirikiano mzuri baina ya vyama vya wafanyakazi na mashirika ya mashinani una uwezo wa kuendeleza kwa ukubwa maadili ya Mkataba wa 182 na athari njema kwa maisha ya watoto.**

## **Jinsi Mashirika ya Jamii yanaweza kutumia Mkataba wa 182 na Pendeleko la 190-Kujihusisha katika mipango ya Kitaifa ya Utendaji.**

### **Utambuliaji wa ni ipi mifumo mibya zaidi ya ajira ya watoto**

Ibara ya 3, aya 3 ya Mkataba wa 182 na sehamu ya pili (II) ya Pendeleko la 190 kuhusu ajira zilizo na hatari, zinatoa fasiri na mifano ya mifumo mibya zaidi ya ajira ya watoto.  
Kazi ya afisi ya ILO/IPEC na ya Mashirika ya

Jamii ulimwenguni, imetambulisha, mifumo mibya zaidi ya ajira ya watoto katika hali nyingi tofauti katika nchi mbali mbali na katika maeneo.

Makundi ya mashirika ya Jamii ni lazima yachukue utaratibu wa kuhakikisha yanajihusisha katika harakati za mashauriano na Serikali. Mashauriano haya yanapaswa kuwa na utaratibu wa kudumu na siyo tu ya utaratibu wa kusudi maalum.

Matukio ya utekelezaji wa CRC, yanadhihirisha kwamba Mashirika Ya Jamii yanapaswa kusisitiza utaratibu huu uruhusu:

- ❖ **Wakati muafaka wa mashauriano na wa kutoa maoni kuhusu nyaraka zinazostahili**
- ❖ **Mbinu ama njia za mawasiliano zilizokubaliwa na uangavu panapowezekana**
- ❖ **Uzingativu wa vikwazo vya rasilmali na hatimaye kutunga mipango inayozingatia vipaumbele**
- ❖ **Mabadilishano ya maeleo kwa utaratibu.**



© ANPPCAN Regional Office

- ❖ **Utambulishaji wa ni ipi mifumo mibya zaidi ya ajira ya watoto.**
- ❖ **Maeleo ya Kitakwimu**
- ❖ **Kupiga kampeni na kuhamasisha**
- ❖ **Kushswishi**
- ❖ **Kanuni za kisheria/ utekelezaji wa 182**
- ❖ **Uondoaji/ulinzi na uunganishaji upya wa watoto na jamii**
- ❖ **Ufuatiliaji wa harakati za ILO**

## 5. TOGO: Uchunguzi kifani.

Serikali ya Togo iliidhinisha rasmi Mkataba wa 182 Septemba 2000. Kutekeleza Mkataba wa 182 kumeleta matatizo fulani ambayo yanahitaji **jithada za pamoja na harakati za aina nyingi** kutoka wote wanaopigania kumaliza mifumo mibaya zaidi ya ajira. Miungano baina ya wenzi katika ngazi za mashinani, maeneo na za kitaifa, ni ya umuhimu. Kwa bahati nzuri, Mkataba huu ni kama mwanzo na turufu ya mwisho iliyo mkononi, kwa wanaojihusisha na mapambano.



© ILO/IPEC Kenya

Mashirika ya raia yanaendelea kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba Serikali ya Togo inahakikisha Mkataba huu unatekelezwa. Cha kipaumbele ni uhamasishaji wa wanaohusika katika jamii (Bunge; vyama vya wafanyakazi; mashirika; mamlaka za kitawala na watoto walioajiriwa) ili kuendeleza utekelezaji unaofaa.

Uhamasishaji umefanywa kwa kutumia **Mkakati Wa Uhamasishaji Wa Kijamii** uliozinduliwa Na “PLAN-International”, Togo na “WAO-Afrique” (Shirika la Togo linaloshughulikia tatizo la ajira ya manyumbani na ulangizi wa watoto). **Wameanzisha mfumo wa kuinua ufahamu na wa maelezo kutumia njia za kuwasiliana za**

**kitamaduni na runinga (televisheni) na pia njia za kujiwasilisha kwa kusema na kwa kuigiza (kama vile michezo ya kuigiza).**

Uhamasishaji unaendelea. Katika mwaka wa 1998 IPEC, kwa maombi ya Serikali, ilifanya utafiti wa hali ya kuishi na kufanya kazi, katika ajira ya watoto, viwandani na katika sehemu fulani nchini Togo. Matokeo yalitumiwa katika mkutano wa **Mazungumuzo ya Kitaifa ya Pande** **Tatu** **kuhusu uidhinishaji wa Mpango wa Taifa wa Utendaji uliofanyika Machi 2000.**

April 2000, kuliandaliwa semina nchini Togo ya kuendeleza Uhushishaji wa **Mashirika ya raia nchini Togo na Ghana** katika utekelezaji wa **Mkataba wa 182**, iliyopangwa na WAO-Afrique na PLAN International, Togo, wakishirikiana na shirika la Kimataifa linalopinga Utumwa (“Anti-Slavery International”).

**Semina hiyo ilihudhuriwa na waakilishi wa Wizara, vyama vya wafanyakazi, baadhi ya mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ngazi tofauti na waandishi wa habari.**

**Watoto waajiriwa walichangia kwa kurekodiwa. Semina hii ilidhamiria kuitisha Mkakati Wa utendaji wa Pamoja wa Kuhakikisha uratibu wa Shughuli katika ngazi zote za uwezo wa utendaji, zikijumuisha za kitaifa na za pande mbili; kufanya kazi pamoja katika utekelezaji wa Mkataba wa 182 wa kuongeza uwezo wa kufanya hivi; na kuongezea nguvu miungano baina ya mashirika ya Jamii yenewe kwa yenewe na baina ya mashirika hayo na Serikali.**

Warsha za Semina hiyo zilizaa makubaliano tofauti ya mapendekezo ya utendaji.

Yanahusisha:

❖ **Kuzindua kikao cha pande mbili cha ubadilishanaji wa maelezo na kuishawishi serikali;**

- ❖ **Kuzianzisha kamati za mashinani za uinuaji wa ufahamu wa watoto wenyewe kwa wenyewe, ndugu na familia zao na kuwafunza mikakati ya mashauriano na watu wazima;**
- ❖ **Kufahamisha umma dhana ya haki za watoo;**
- ❖ **Kutia moyo nia ya kisiasa katika ngazi ya kiserikali na ushirikiano baina ya serikali na Mamlaka za Huduma za Uhamiaji.**

Mwisho, wazo la **Bunge la watoto** la kupendekeza na kuzungumzia masuala haya limezingatiwa nchini Togo. Bunge la Togo kwa sasa linawachagua watoto kutoka kiwango cha maeneo ambao watashiriki katika Bunge za watoto za siku za usoni!

## 6. Shirika la undugu la kenya

Mojawapo ya malengo ya mpango wa IPEC nchini Kenya, ilikuwa ni kuwaondoa watoto kutoka kazini, hasa wale waliokuwa katika aina mbaya zaidi za ajira ya watoto. Kisha kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida na kuwaunganisha tena na familia zao. Huu ulikuwa mpango wa muda mfupi. Lengo kuu la mpango wa nchi katika kipindi cha 2000

– 2001 ilikuwa ni kupambana na aina mbaya zaidi za ajira ya watoto, hasa huduma za nyumbani, kazi za barabarani na ukahaba wa watoto.

Mwezi wa Julai mwaka wa 2000 shirika la undugu la Kenya, chini ya mpango wa IPEC ilidhamiria kuwaondoa watoto 800 waliokuwa wakifanya kazi barabarani na kuwasaidia kujikimu. Kati ya hao, watoto 400 (wavulana 240 na wasichana 160) wa miaka 15 – 18 wangejiunga na mipango

ya kutoa mafunzo ya kazi za kiufundi. Wengine 200 wa umri wa miaka 8—12 wangeunganishwa tena na familia zao na kusaidiwa kuingia shulen. Wale ambao tayari walikuwa wamepata mafunzo ya kiufundi (wavulana 30 na wasichana 20 wa umri wa miaka 16 – 18) wangesaidiwa kupata ajira. Undugu pia ilidhamiria kutoa mikopo ya kuanzisha biashara ndogo kwa wazazi 100. Mwisho, watoto 100 walipangiwa kupata huduma za afya za kimsingi.

Kufikia Oktoba mwaka wa 2001 shirika la Undugu ilikuwa limewaondoa watoto 100 kutoka barabarani na kuwapeleka kwenye mafunzo ya kiufundi (wavulana 66 na wasichana 34). Watoto 887 badala ya 800 walikuwa wamepokea huduma za afya. Mpango wa utendaji wa Undugu unadhihirisha jinsi mipango ya utendaji ya IPEC nchini Kenya ilivyomakinika. Pia, inadhihirisha ufanisi, kwa kuwa katika kipindi kifupi watoto wengi wamehudumiwa.

# **PROTOKALI HAIRI ZA MAPATANO YA HAKI ZA WATOTO**

**Aina mbaya zaidi za ajira ya watoto kwa sasa ni mambo yaliyopigwa marufuku kisheria kimataifa. Mwanzo wa 2000, nyaraka mbili zaidi zilitungwa ili kuongezea mapatano baina ya Serikali kuhusu haki za watoto. Serikali zinaweza kutia saini na kuidhinisha rasmi protokali hizi kama zinavyoufanya Mkataba Mkuu. Mashirika mengi yanashawishi serikali zao kufanya hivi.**

**Mapatano haya ni Protokali za Hiari za Mkataba wa Haki za Watoto. Protokali moja ni ya Uhusishaji wa watoto katika Mapigano na ile nyingine ni ya Uuzaji, Ukahaba na ponografia. Harakati za kumaliza hali mbaya zaidi za watoto wanajeshi, zinafanywa ulimwenguni wote na zinafaidika kutopteka na sheria hii mpya.**

## **SEKTA ISIYO RASMI.**

**Lililosaulika kwa urahisi ni idadi kubwa ya watoto wanaofanya kazi katika sekta isiyo rasmi. Hii ni ajira iliyovuka mipaka ya udhibiti wa kawaida wa kanuni za ajira: haswa kazi zisizoonekana zilizo manyumbani, katika familia na mashambani, katika vyumba vya kinyuma-nyuma ama mitaani. Pia, ni unyonyaji ambao kwa kawaida hauhusishwi na ajira rasmi; kama ukahaba, uombaji na ulanguzi wa madawa ya kulevya.**

**Njia maalum za kuwafikia hawa watoto zinahitajika kwa haraka na harakati za kuanzisha njia hizi ni lazima ziwe katika Mipango ya Utendaji ya Kitaifa. Kwa kawaida, watoto wengi kama hawa wamechukuliwa kuwa wagumu kufikiwa, ama suala lililoachiwa familia kuamua. Hata hivyo, mifano ya maendeleo ya mabadiliko ya mitazamo ya ajira ya watoto kama wafanyakazi wa nyumbani ni dhihirisho kuwa kupambana na matatizo haya si jambo lisiloweza kufaulu.**

## **Maelezo ya Kitawakwimu.**

Mkusanyiko wa maelezo ya kitawakimu yaliyo sahihi ni wa umuhimu kwa mipango ya utendaji ya Kitaifa iliyo muafaka na iliyojitosheleza. Makundi yanayo weza kufikia maelezo haya yanapaswa palipo na uwezekano:

- ❖ **Kufanya kazi kwa kushirikiana na bodi rasmi iliyo na wajibu wa kutaja wazi na kukusanya data ama kupitia njia nyingine na kuwasilisha maelezo yao**
- ❖ **Kuhakikisha kuwa ukaguzi unafanyiwa tawakimu za serikali na kutaja wazi malalamiko yao inapojitokeza kuwa tawakimu hizo hazifikiani na ukweli wa mambo**
- Kutia Serikali moyo wa kutekeleza taratibu za usajili unaofaa wa kuzaliwa kwa watoto, kuambatana na Pendekeso la 190.**
- ❖ **Kuahakikisha kuwa data iliyokusanywa inagawanywa kulingana na umri na jinsia.**

## **Kupiga Kampeni na Kuinua Ufahamu.**

Jambo la umuhimu zaidi la kuchangia kufaulu kwa utekelezaji wa Mikataba hii ni kuungwa mkono na Jamii kwa dhamira ya hiyo mikataba. Shughuli zilizopangwa za kuifahamisha umma ni muhimu. Kupitia wanachama, makundi ya kidini, ya wanawake, ya walaji na Mashirika Ya Jamii ya mashinani, yaliyo na uwezo wa kufikia na kuathiri mitazamo ya watu binafsi na jamii kwa jumla:

- ❖ **Yainue ufahamu kuhusu hali zisizokubalika za wale watoto**

**ambao Mikataba hii inadhamiria kuwalinda, kwa mfano kupitia warsha na michezo ya kuigiza**

- ❖ **Kunamasisha uungaji mkono uliopendwa na wengi kwa mabidiliko katika maisha ya hao watoto**
- ❖ **Kutumia uungaji mkono kusositiza uidhinishaji wa mikataba na njia muafaka za utekelezaji**
- ❖ **Kutia moyo umuhimu wa kuelewa haki za kisheria za watoto na watu wazima na kutafsiri nyaraka zinazostahili kwa lugha tofauti na zinazoeleweka**
- ❖ **Kuimarisha mapatano ya pamoja yaliyozinduliwa na Mikataba hii ya kupambana na mifumo isiyokubalika ya ajira ya watoto.**

## **Ushawishi**

Ushawishi ni jambo la muhimu linalotumia kampeni za kuathiri watu fulani walio katika nafasi za mamlaka na uwezo. Mashirika katika ngazi za chini na kitaifa yanaweza kuelekeza kampeni zao za kuinua ufahamu kwa watu walio na uwezo wa kuathiri mawazo na maoni ya jamii na sio tu wanasiasa na maafisa wa umma peke yao. Yanapaswa pia kulenga:

- ❖ **Mamlaka zilizowajibika katika utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya utendaji na pia mamlaka za kisheria**
- ❖ **Wanasiasa wa mashinani na wa Kitaifa na pia wizara zinazostahili**
- ❖ **Viongozi katika jamii**
- ❖ **Wanahabari**
- ❖ **Polisi na Ofisi zingine za utekelezaji wa Sheria**

- ❖ **Mashirika mengine ambayo kazi yao inastahili kama vile ya elimu na afya**
- ❖ **Mashirika ya kimataifa na kimaeneo**
- ❖ **Serikali za kigeni na Biashara ili kutia shinikizo kwa serikali na baina ya biashara zenyewe kwa zenyewe.**

## **Kanuni za Kisheria / Utekelezaji wa Mkataba wa 182.**

Tume za Kitaifa za Haki za kibinadamu, wanaharakati wa mashinani wa kutetea haki za kibinadamu na mashirika ya mawakili kwa umahususi, makundi ya haki za kibinadamu na tume zinaweza kuwa na umahiri wa:

- ❖ **Kushawishi serikali kuhakikisha kwamba miwachano kati ya sheria zilizopo na Mkataba wa 182 inatatuliwa**
- ❖ **Kushawishi ili mifumo mibaya zaidi ya ajira kufanywa kuwa makosa ya jinai**
- ❖ **Kutangaza kesi kuhusu ukiukaji wa sheria hizi**
- ❖ **Kusisitiza juu ya taratibu za sheria zinazoleta kesi hizi kwa haraka**
- ❖ **Kufuatilia maendeleo ya kesi ili kuhakikisha adhabu zinazofaa zinatolewa dhidi ya watu wanapopatikana na hatia**
- ❖ **Kushawishi ili kuwe na rejestra ya kitaifa ya wanaotenda makosa kama haya**
- ❖ **Kuhakikisha kuwa maelezo**

yanayohusikana na kesi za ajira ya watoto ambazo ni hatia yanapelekwa kwa mashirika ya jamii na pia yale ya kimataifa panapostahili.

## **Uondoaji / ulinzi na ukarabati na uunganishaji upya na jamii.**

Mipango ya kitaifa ya utendaji ni lazima idhihirishe njia za uondoaji, ulinzi, ukarabati na uunganishaji upya wa watoto walio katika mifumo mibaya zaidi ya ajira.(Ibara ya 7, aya ya 2 ya M182). Mahitaji ya mtoto ya umuhimu zaidi yanapaswa kuzingatiwa katika mipango hii, kuambatana na ibara ya 3 ya CRC. Mashirika yanayojihusisha na masuala haya kwa sasa yako na miradi inayoendelea vizuri na kutoa uzoefu ambao unaweza kuzionyesha serikali harakati zilizo faulu ambazo zinaheshimu kikamilifu haki za watoto na kuzingatia maoni yao.

Mara nyingi, miradi hii hujaribu kuzuia haja ya watoto ya kufanya kazi kupitia upunguzaji wa umaskini. Hata hivyo, hali ya watoto walio katika ajira mbaya zaidi za unyonyaji, mipango ya kuwaondoa, kuwakarabati na kuwaunganisha upya na jamii baadaye, inahitajika. Mipango inayopitishwa kwa madhumuni kama haya inajumuisha:

- ❖ **Kuanzisha nambari za simu za dharua za kuripotia kesi za ajira za watoto;**
- ❖ **Uinuaji wa ufahamu wa haki za wafanyakazi walio katika hali za hatari, kwa mfano kwa kutumia redio na runinga;**
- ❖ **Mikakati ya pamoja baina ya watoto, familia, mashirika na mamlaka zinazostahili kama inawezekana, ya kuwaondoa watoto palipo haja na ambapo**

- ❖ **mapato mengine yanaweza kupatikana.**
- ❖ **Kuwapa watoto ulinzi. Kama vile maskani za usalama wa dharura, lishe na mavazi, utunzaji wa kimatibabu na ushauri.**
- ❖ **Nafasi za kupata elimu na masomo ya ufundi, iwe ya kirasmi amaisiwe ya kirasmi, na umahiri wa maisha.**
- ❖ **Kuwapatia nafasi za burudani na kujifunza maadili ya kijamii.**

## **Njia za ILO za Ufutiliaji.**


ILO iko na njia kadhaa za kufutilia hatua za Serikali za uidhinishaji rasmi na utekelezaji wa Mikataba. Njia hizi ni kama:

- ❖ **Ripoti za Vipindi:**  
Serikali zinashurutishwa kutoa ripoti za vipindi kwa ILO kuhusu jinsi walivyotumia mikataba ya ILO zilizoidhinisha. Ripoti hizi huchunguzwa na kamati ya wataalamu ya ILO ambayo hutayarisha ripoti iliyo na uamuzi wa kamati yenewe.
- ❖ **Kamati ya Mkutano:**  
Kulingana na ripoti ya Kamati ya Wataalamu, wakati wa Mkutano Wa Kimataifa Wa Ajira wa kila mwaka, ukiukaji wa kanuni za Mikataba unaojitokeza katika hiyo ripoti, huzungumziwa katika kikao kikuu. Wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi hupendekeza kesi zinazopaswa kuchunguzwa.
- ❖ **Mikataba ya Msingi:**  
Kuna mikataba minane (8) ya ILO ambayo huzingatia maadili manne (4) ya msingi zaidi na haki ajirani. Serikali zote zilizo wanachama wa ILO hujifunga zenyewe, hata kama hazijaidhinisha mkataba , kuheshimu,kuendeleza na kutekeleza kanuni ya uondoshaji wa ajira ya watoto ( na kanuni nyiginezo).
- ❖ **Kuhusu ajira ya watoto:**  
Mikataba inayostahili ni Nambari 138 kuhusu Umri Mdogo Zaidi na nambari 182. Kama Serikali haijaidhinisha mikataba hii miwili, ILO itaiomba itoe ripoti inayoeleza mabadiliko yoyote katika Sheria na Utendajji katika sekta hii. Mashirika ya waajiri na waajiriwa yanaweza kutoa maoni yao kuhusu ripoti hizo.
- ❖ **Ripoti ya Ulimwengu:**  
Kila mwaka masuala ya ILO hutoa ripoti kuhusu mojawapo ya maadili manne. Kuanzia 2002, kila miaka minne, Ripoti ya Ulimwengu ya Ajira ya Watoto itagusia hatua zilizopigwa ulimwenguni kote; katika nchi zilizoidhinisha na zile ambazo hazijaidhinisha Mikataba Ya182 na 138. Ripoti hii pia itatathmini kazi iliyofanywa na ILO ulimwenguni kuhusiana na mikataba hii.

Njia inayofaa kwa mashirika ni kuchangia maoni yao kwa njia hizi na kupitia kushirikiana na mashirika ya waajiriwa na ya waajiri, katika ngazi zote.

## 7 Shirika la ustawi wa watoto la Kenya

Shirika la Ustawi wa Watoto la Kenya ni shirika lisilokuwa la kiserikali ambalo lina uwakilishi wa mashinani. Shirika hili lilifaidika kutokana na mpango wa IPEC nchini Kenya. Tangu lianzishwe mwaka wa 1992, shirika la Ustawi wa watoto la Kenya lilianza kutekeleza mipango ya IPEC katika sehemu za Bungoma, Mombasa



© ILO/IPEC Kenya

na Nairobi. Sehemu hizo ndizo zilizotambuliwa kuwa na watoto waliokabiliana na shida. Baadhi ya watoto hao walirudishwa shulen, wengine wakapewa mafunzo ya kazi na wengine wakaunganishwa tena na familia zao baada ya kushauriwa. Shirika hili limefanya ukaguzi wa watoto wa barabaranii mjini Nairobi mwaka wa 1994. Pia limewasaidia wavulana na wasichana 544 kuingia shulenii katika sehemu zote tatu ambapo shirika hili limekuwa likifanya kazi.

Lengo la Shirika la Ustawi wa Watoto la Kenya ni kuwasaidia watoto wa barabaranii, hasa wasichama walioingia katika ukahaba na walioolewa mapema. Iligunduliwa kwamba wakati huo hakukuwa na mipango yoyote iliyolenga wasichana wa barabaranii na kwamba kulikuwa na haja ya kuwaondoa kutoka mazingira mabaya ya barabaranii. Mpango huu

ulijulikana kama Nyumba ya Uokoaji ya Amani (Rescue Peace House). Watoto wengi wa barabaranii walidhulumiwa. Kulingana na taarifa juu ya watoto waliookolewa, asilimia 70 walikuwa na magonjwa yanayoambukizwa kuitia ngono (STD's) na mmoja alikuwa na ukimwi. Hii inadhihirisha umuhimu wa mpango huu.

Kituo cha kuokolea watoto kilikuwa mahali pa muda pa usalama kwa wasichana walitolewa barabaranii. Wasichana hao walipangiwa kupewa malazi, chakula, nguo, huduma za afya na ushauri. Ilitarajiwa kwamba wangekaa katika kituo kwa muda wa wiki 3 – 6 na baada ya hapo wangepelekwa kwa wazazi wao na kisha wajunge na shule au mafunzo ya kazi.

Malengo ya mradi:

- ❖ Kuzidisha elimu na huduma za afya kwa wasichana wa barabaranii.
- ❖ Kuwaunganisha wasichana wa barabaranii au waliokuwa wakifanya kazi na wazazi/walezi wao.
- ❖ Kukadirika athari za uokoaji wa wasichana wa barabaranii na familia zao.
- ❖ Kuanzisha mfumo wa ushirikiano mionganii mwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayoshughulikia wasichana wa barabaranii.

Shirika la Ustawi wa Watoto la Kenya lililenga kuwaokoa watoto 50 katika kipindi cha kwanza cha mradi. Kituo kiliendeshwa na muuguzi aliyehitimu akiwa mwangalizi, msimamizi wa nyumba, wafanyikazi wa huduma za jamii na wasaidizi. Mratibu wa mradi aliwatembelea wafanyikazi na kushauriana nao mara kwa mara. Taarifa juu ya kila msichana zilihifadhiwa. Wazazi waliarifiwa mara tu watoto walipokuwa tayari kurudi nyumbani. Hali ya nyumbani ilikadiriwa ili kubainisha mahitaji yao na baadhi ya wazazi walisaidiwa na mradi kuanzisha shughuli za kuleta mapato. Wengine walielekezwa kwa mashirika mengine ya kutoa msaada. Wakiwa katika kituo, wasichana walifunza kusoma na kuandika. Baada ya kurekebishwa tabia, wasichana walifunzwa

kusoma na kuandika. Baada ya kurekebishwa tabia, wasichana walifunzwa kazi wakawa wanaweza kuwijiri wenyewe au kubuni kazi na kuwa waajiri.

Changamoto zilizohusika ni kama vile kuboresha afya ya wasichana. Hii ingerhisisha kazi ya kuwarekebisha. Pia kulikuwa na tuhuma za majirani. Jambo lingine ni kwamba wasichana walichukua muda mrefu kutoka katika kituo, hivyo kuufanya mpango wa muda mfupi wa kuwaokoa kuwa wa muda mrefu. Haya yaliufanya mradi kuwa ghali. Mara nyingine utaratibu wa kupata pesa ulikuwa mrefu. Jambo hili lilifanya shughuli ya kuendesha kituo kuwa ngumu.

Nyumba ya Amani (Peace House) ni wazo zuri kwa vile ilizingatiwa kwamba watoto wanahitaji mahali ambapo wanaweza kukaa kwa amani, kuwaza, kushauriwa, kupata huduma za afya, kupata mahitaji yao ya kimsingi na kupertia mchakato wa kuponywa.

## 8. Kituo cha sinaga cha wanawake na ajira ya watoto

Kituo cha SINAGA kilianzishwa kama shirika lisilokuwa la kiserikali mwaka wa 1993 kuwasaidia wanawake waliopondwa na pia wahalifu. Vilevile shirika hili lilifaa kushughulikia suala la watoto walio katika huduma za kinyumbani mwaka wa 1995.

Hatua mojawapo iliyochukuliwa na Sinaga ni kujaribu kuwazuia watoto walio katika huduma za kinyumbani wasiingie katika ukahaba. Hili lilifanya kwa kuwafunza wasichana kazi fulani za kiufundi na pia kuwasaidia wale wenye umri mdogo kurudi shulenii.

Malengo ya mradi yalikuwa:

- ❖ Kutoa mafunzo ya kazi ya awali pamoja na misingi ya kusoma na kuandika kwa wasichana waliokuwa katika huduma za kinyumbani kama wafanyikazi.

- ❖ Kuelimisha jumuiya juu ya ubaguzi wa kijinsia unaopelekea wasichana kuajiriwa katika huduma za kinyumbani.
- ❖ Kutoa ushauri na mafunzo ya kazi kwa wasichana wafanyao kazi za kinyumbani na kutafuta njia za kushirikiana na jumuiya katika harakati za kupambana na ajira ya watoto.

Mpango huu unaendelea katika mtaa wa Kariobangi North na unalenga wasichana wa umri wa kati ya miaka 8 na 16 ambao wameajiriwa kufanya kazi za kinyumbani au wale ambao wamekosa kuhudhuria shule kwa sababu ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi ili kusaidia familia zao.

Kazi za kiufundi ambazo zinafunzwa ni kama vil emapishi, ufundi cherahani na upigaji chapa. Wasichana pia wanashauriwa na kupewa usaidizi wa kisheria kulingana na mahitaji yao. Kituo cha Sinaga kilikuwa kimesajilisha watoto 200 ambao wanakwenda hapo kwa zamu, yaani asubuhi na alasiri. Hivi ni kwa sababu wengi wa watoto hao walikuwa bado wameajiriwa. Kituo cha Sinaga kimefaulu kuondoa asilimia 5 ya watoto hawa kutoka kazini.

Idadi kubwa ya wasichana hutumiwa vibaya na waajiri wanaofanya mapenzi nao. Kwa sababu hii, wengi wao wameambukizwa kila aina ya magonjwa yanayosambazwa kupertia ngono. Kwa hivyo kituo cha Sinaga kinafikiria kuanzisha kituo cha uokoaji ili kuwasaida wasichana hawa na wengine ambao wameachwa mayatima kutokana na janga la ukimwi.

Mafunzo ambayo wasichana hawa wanapata ndiyo njia ya kuwaepusha na maisha ya kiutumwa. Ufundu ambao wasichana hawa wanapata unawasaidia kuondokana na udhalimu wa kuishi maisha ya kikawaida kama watu wengine. Mradi huu umefaulu kuwarekebisha kitabia zaidi ya watoto 1000 tangu uanzishwe. Zaidi ya watoto 200 wamepitia mafunzo ya kusoma na kuandika na wengine 778 wamepitia katika mafunzo ya kiufundi.

Idadi ya watoto waliookolewa kutokana na dhuluma mbalimbali ni dalili ya ufanisi wa mpango huu. Hata hivyo, inaweza pia kuwa dalili ya ukubwa wa tatizo lililopo. Lakini ukweli ni kwamba idadi kubwa ya wasichana hawa wamezuiwa kuingia katika ukahaba. Waliofuzu kutoka Sinaga wameingia katika kujajiri, huduma bora zaidi za kinyumbani, asasi za uandazi chakula na wengine kurudi shuleni.

Sinaga ndio mradi wa pekee kufikia sasa ambao unashughulika na ajira ya watoto ambayo ni ngumu zaidi kutambulika ambapo watoto wanadhalimiwa na watu wasioadhibiwa.

## 9. Jukumu la muungano mkuu wa wafanyakazi (Cotu-k) katika kuondosha ajira ya watoto

Serikali ya Kenya ilitia sahihi mkataba wa Uelewano na Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi (ILO). Lengo lake ni kuondosha ajira ya watoto nchini Kenya kupitia mpango wa Kimataifa wa ILO wa Kuondosha Ajira ya Watoto (IPEC). Serikali imeldhinisha maagano nambari 105 juu ya Ajira ya kulazimishwa, Maagano nambari 138 juu ya Umri wa Chini Zaidi, na karibuni, Maagano nambari 182 yanayolenga kuondosha aina mbaya zaidi za ajira ya watoto.

Vyama vya wafanyakazi vina jukumu muhimu hapa. Hivi ni kwa sababu:

### (i) Ajira ya watoto inadhoofisha mapato ya wafanyakazi ambao ni watu wazima.

Waajiri hupendelea kuwaajiri watoto ambao ni rahisi kunyonya na ambao ni rahisi kuajiri na kufuta kazi. Watoto pia wanachukuliwa kuwa watiifu na dhaifu hivi kwamba hawana uwezo wa kukataa kufanya kazi zenye hatari, dhuluma na malipo duni.

### (ii) Matendo dhidi ya ajira ya watoto yanahusiana na uwezo wa vyama vya wafanyakazi kutoa mafunzo na elimu.

Kuondoa ajira ya watoto na kuhakikisha elimu kwa wote ndiyo malengo ya vyama vya wafanyakazi. Nguvu ya vyama vya wafanyakazi inatokana na wafanyakazi wanaofahamu haki zao na jinsi wanavyoathiriwa na sekta nyingine za jamii.

### (iii) Vita dhidi ya ajira ya watoto vinaweza kutumiwa kuvipa nguvu zaidi vyama vya wafanyakazi.

Mipango ya uondoaji ajira ya watoto iliyofikiriwa vizuri inajumlisha ujenzi wa uwezo wa mashirika ili yaweze kuendesha mipango yao. Uondoaji wa ajira ya watoto na uboreshaji wa ajira ya watu wazima unawapa nguvu zaidi wanachama wa vyama vya wafanyakazi. Pia vyama hivi vinapata wanachama zaidi.

### (iv) Masuala ya ajira ya watoto ndiyo kiini cha harakati za vyama vya wafanyakazi.

***Kupitia kwa uwezo wao, vyama vya wafanyakazi hupigana na dhuluma, hupinga unyonyaji, hutetea mazingira bora ya kufanya kazi na uondoshaji wa ajira ya watoto.***

Kwa matendo yake na kwa kushirikiana na mashirika mengine yasiyokuwa ya kiserikali, COTU imefaulu katika: Kuwaelimisha wafanyakazi juu ya athari za ajira ya watoto, kubuni kamati za Jumuiya za Ajira ya Watoto zinazofutilia matukio ya aina mbaya zaidi za ajira ya watoto, kuandikisha wanachama zaidi ili kuvipa nguvu zaidi vyama vyetu, kuleta pamoja wazazi (wafanyakazi) katika makundi ili kuanzisha shughuli za kiuchumi, kuondoa watoto kutoka kazini na kuwapeleka shuleni.

## Changamoto

- (a) Uwezekano wa kuendeleza mipango ya uondoaji wa ajira ya watoto katika hali ya umaskini.
- (b) Umilikaji wa mradi pale ambapo jumuiya zinahitaji kuelimishwa ili ziweze kufahamu kwamba ndizo zinazomiliki mradi wa ajira ya watoto na sio wafadhili au wasaidizi.
- (c) Mipando ya Marekebisho ya Kimundo (SAPS) ambayo inazifanya huduma za kijamii kuwa ghali na zisizoweza kugharamiwa na maskini.
- (d) Ukimwi unaoacha mayatima na wengine wanaoathiriwa kushindwa kujikimu na hivyo kuingia katika ajira ya watoto.
- (e) Ukosefu wa ajira na ustaa fishwaji unaopelekea baadhi ya familia kuwategemea watoto kujikimu.
- (f) Umaskini unaopelekea kuzuka kwa watoto wanaohitaji utunzaji maalumu wakiwemo watoto walioajiriwa.

## Hitimisho

1. Tatizo la ajira ya watoto linajitokeza zaidi katika kilimo cha biashara. COTU kikishirikiana na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali pamoja Chama cha Kitaifa cha Walimu cha Kenya, kilianzisha mpango wa kitaifa wa ajira ya watoto. Tatizo hili linahitaji ushirikiano wa wahusika wengi ili kuweza kutatuliwa. Ni jambo zuri kwamba Kenya imeweka sheria za waziwazi zinazokataza ajira ya watoto. Uangalifu na usambazaji habari kuhusu tatizo hili unahitaji kuendelezwa katika jumuiya zetu.

### 10. Halmashauri Ya Tanzania Ya Maendeleo Ya Kijamii (Tacosode): Tajariba Katika Kushughulikia Matatizo Ya Ajira Ya Watoto

Tangu ijiunge na Mpango wa Kimataifa wa Uondoshaji wa Ajira ya Watoto wa ILO (Shirika la Kimataifa la Wafanyikazi). Tanzania imepiga hatua kubwa katika kupambana na ajira ya watoto hasa aina mbaya zaidi za ajira. Imefanya hivi kwa kutumia mbinu mbalimbali na pia

kuwahuisha watu wengi ambao sasa wanachangia pakubwa katika vita dhidi ya ajira ya watoto.

Serikali ya Tanzania imeidhinisha Maagano nambari 138 mwaka wa 1998 na Maagano nambari 182 mwaka wa 2001. Serikali pia imekuwa ikirekebisha sheria na sera zinazohusiana na ajira ya watoto kwa lengo la kubuni sera ya kitaifa ya ajira ya watoto.

TACOSODE ni mojawapo ya wahusika muhimu katika ajira ya watoto nchini Tanzania na imeshiriki katika mpango wa ILO/IPEC. Imefanikiwa kuvutia wanachama wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika utekelezaji wa mipango ya matendo kwa kutoa mafunzo juu ya ajira ya watoto katika kazi zenyet hatari. Tangu 1998 TACOSODE imefanya kazi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ya mashinani katika maeneo saba ya nchi, kwa lengo la kuimarisha iutendaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali na jumuiya kuhusiana na ajira ya watoto katika huduma za kinyumbani, kilimo cha biashara na ukahaba.

Nchini Tanzania, watoto walioajiriwa hupatikana katika kilimo cha biashara hasa kuhusiana na mazao kama vile majani chai, kahawa, tumbaku kazi za kinyumbani na ukahaba.

Umaskini, ukimwi, kuvunjika kwa maadili, matatizo ya ndoa, uzazi usiowajibika, mila na desturi fulani ni baadhi ya visababishi vya ajira ya watoto nchini Tanzania.

### Baadhi ya shughuli ambazo TACOSODE imeshiriki ni kama vile:

- ❖ Matembezi ya dunia nzima dhidi ya ajira ya watoto nchini Tanzania mwaka wa 1997 na pia mafunzo na maelekezo juu ya ajira ya watoto katika kazi zenyet hatari kwa mashirika 15 yasiyo ya kiserikali kwa lengo la kuyaelimisha na kuya elekeza juu ya ajira ya watoto. Haya ni kwa lengo la kuyawezesha mashirika yanayohusika kuwa na mipango juu ya ajira ya watoto

ambayo inaingiliana vizuri na shughuli zao za kila siku.

- ❖ Uteuzi wa mbia mionganoni kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Ilibidi mashirika haya yazingatie haki za watoto, yawe na tajiriba ya kufanya kazi katika kiwango cha jumuiya na yawe tayari kushiriki katika masuala ya ajira ya watoto.  
Mwisho, yawe na uwezo wa kuendeleza shughuli za mradi.

#### Kuendeleza Utendaji wa Jumuiya Dhidi ya Ajira ya Watoto

Kazi iliyofanywa ilihusu utambulishaji wa watoto waliofaa kushauriwa na kuelimishwa, baadhi yao wakiwa wafanyakazi, mazungumzo na watoto wafanyakazi na familia zao, kuwarudisha shuleni watoto au kuwaelekeza katika shughuli za kiuchumi kama walikuwa wamepita umri wa kurudi shuleni.

TACOSODE pia ilizisaidia familia za watoto hawa kufunga akaunti ya mikopo ambayo ingesaidia katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi. Waliofaidika zaidi walikuwa wanawake.

Mikakati muhimu iliyotumiwa ilikuwa ni kama vile kuwashirikisha wanachama wa mashirika yasiyo ya kiserikali wilayani kama wabia. Pia kudumisha ubia na ushirikiano na watu kutoka sekta mbalimbali. Jambo muhimu katika mpango huu ni kuanzisha njia za ushirikiano baina ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na serikali za mitaa na serikali kuu. Mwelekeo huu ulileta ungaaji mkono kisiasa katika kiwango cha wilaya na pia mazingira muafaka kwa kukua kwa ushirikiano pamoja na sekta mbalimbali. Uingizwaji wa mpango katika mipango ya wilaya uliwezekana kwa sababu ya kushiriki kwa ofisi za wakuu wa wilaya katika mpango. Viongozi kutoka halmashauri mbalimbali pia walishiriki katika warsha zote za upangaji.

#### **Mafanikio ya Mpango wa Sasa.**

Kulingana na mpango, idadi ya familia maskini zilizolengwa ilikuwa 250 kabla ya mwisho wa mwezi Machi 2002. Kufikia mwezi Agosti 2001 mpango huu ulikuwa umezipa familia 191 msaada wa kifedha. Idadi hii iliwalishwa asilimia 76.4 ya familia zilizolengwa. Watoto 239 wafanyakazi pia walipata msaada wa kimasomo katika awamu ya kwanza ya mpango. Hii ni asilimia 23.9 ya watoto wafanyakazi. Msaada waliopata unajumlisha kurudishwa shuleni, mafunzo ya kiufundi katika nyanja kama vile ufundi cherahani, urembeshaji nguo, uunganishaji vyuma, uendeshaji gari, uandaaji chakula, utiaji nakshi, n.k.

*kuhimiza kushiriki kwa wote katika mapambano dhidi ya aina mbaya zaidi za ajira ya watoto*

Mwaka wa 1992 Shirika la ANPPCAN liliungana na serikali kupitia Wizara ya Leba na Ustawi wa Wafanyakazi kushiriki katika mpango wa ILO/IPEC uliokuwa umeanzishwa nchini Kenya. Baadaye ANPPCAN ilianzisha jitihada zake ambazo zilijulikana kama "kuhimiza kushiriki kwa wote katika kupambana na aina mbaya zaidi za ajira ya watoto". Nia ya ANPPCAN ilikuwa ni kupambana na ajira ya watoto nchini Kenya kupitia harakati za kupinga. Malengo yake yalikuwa:

- ❖ Kuendeleza mahusiano ya sekta mbalimbali mionganoni mwa idara za serikali na washika dau wengine na kuimarisha Kamati za Wilaya za Kutoa Ushauri Juu ya Watoto.
- ❖ Kuendeleza kushiriki kwa watoto katika masuala yanayowaathiri shuleni na katika kiwango cha jumuiya na pia kupunguza idadi ya watoto ambao wanaingia katika ajira.
- ❖ Kupunguza idadi ya watoto walio katika aina mbaya zaidi za ajira ya watoto.

## **Kuendeleza Ushirikiano wa Sekta Mbalimbali katika kukabiliana na Ajira ya Watoto.**

ANPPCAN ilibainisha kwamba ukosefu wa ushirikiano uliathiri ufanisi wa vita vya kukomesha ajira ya watoto nchini Kenya. Kwa sababu hii mpango wa ANPPCAN wa ajira ya watoto ulianza kufanya kazi pamoja na wahusika wengine ili kuimarishe mkakati wa ushirikiano katika kupambana na ajira ya watoto. Kwa njia hii, uendeshaji wa shughuli za pamoja utililiwa nguvu. Kwa mfano kufungua na kuendesha akaunti za benki za pamoja, uendeshaji wa pamoja wa mipango ya mafunzo, n.k.

Katika kuimarishe mkakati wa ushirikiano, ANPPCAN ilitambua Kamati za Wilaya za Kutoa Ushauri Juu ya Watoto kama chombo muhimu katika kiwango cha wilaya ambacho kilihitaji kuimarishe. Hata hivyo, kutokana na ukubwa wa kamati hizi, suala la kutokutana mara kwa mara na pia wakuu wa wilaya ambao ndio wenye kiti wa kamati kuwa na shughuli nyingi sana, ANPPCAN iliamua kuunda kamati nyingine za wilayani. Kamati hizi (DCLC) zili kuwa kamati ndogo za kufanya kazi na Kamati za Wilaya za Kutoa Ushauri Juu ya Ajira ya Watoto (DCAC). Kamati hizi mpya zili kuwa na wawakilishi kutoka idara za serikali, mashirika ya kidini, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wahusika wengine katika masuala ya watoto wilayani.

Majukumu ya Kamati ni:

- ❖ Kutekeleza shughuli za ajira ya watoto
- ❖ Kusaidia shule kuanzisha miradi ya kuleta mapato.
- ❖ Kutoa mafunzo na kuendesha semina, warsha na mikutano
- ❖ Kubuni mipango ya kazi kwa wilaya na kukagua maendeleo yake
- ❖ Kubuni kamati za ajira ya watoto katika viwango vya tarafa na lokesheni.
- ❖ Kutafuta na kutumia raslimali.

- ❖ Kuhakikisha kwamba kuna ushirikiano wa sekta na mionganoni mwa washika dau na pia kusambaza habari juu ya shughuli za kiuchumi zinazohusiana na ajira ya watoto, n.k
- ❖ Kuitisha mikutano juu ya ukaguzi wa shughuli za kuleta mapato.
- ❖ Kutayarisha ripoti za maendeleo ya shughuli za kuleta mapato na shughuli nyingine kuhusiana na ajira ya watoto.
- ❖ Kueneza ufahamu juu ya ajira ya watoto.
- ❖ Kufuatilia na kutathmini shughuli za kuleta mapato.

### **Kupunguza Idadi ya Watoto Wanaojiunga na Soko la Ajira**

Lengo hili lilitekelezwa kupitia kuimarishe ufahamu na pia usaizidi kwa watoto amba walikabiliwa na hatari ya kutolewa shulen. Mwanzoni, jumuiya ilishirikishwa katika kuimarishe ufahamu, kutambua aina za ajira ya watoto ziliaohusika na kukubaliana juu ya mkakati wa kukabiliana nazo.

Semina katika kiwango cha wilaya ziliendeshwa. Zilihusisha idara za serikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, makanisa, mashirika ya jumuiya na viongozi wa elimu ya uraia. Katika kiwango cha jumuiya, wazazi, walimu na watoto wa shule. Lengo lili kuwa ni kuwaelimisha juu ya ajira ya watoto na pia kutafuta maoni yao juu ya njia za kukabiliana na tatizo hili.

### **Maandalizi ya Kufikia Makubaliano**

ANPPCAN ilihusika katika shughuli za Matembezi ya Dunia Nzima dhidi ya ajira ya watoto pamoja na nchi nyingine za Kiafrika zitumiazo lugha ya Kiingereza. Kwa kutumia njia ya ushirikiano wa sekta mbalimbali katika viwango vya kitaifa na wilaya shughuli zilipangwa. Mikakati mbalimbali ilitumiwa ikiwa ni pamoja na matembezi yaliyohusisha umma, vyombo vya habari na mabango. Chochote kilichotokana na shughuli hizi kiligawanywa mionganoni mwa washika dau wote.

Shughuli za kuleta mapato zilitambuliwa kama njia moja ya kuanzisha msingi wa raslimali katika kiwango cha shulenii ili kuwasaidia watoto maskini na kupunguza ada za shule. Hii ilitokana na kutambua kwamba shule zina raslimali nyingi kama vile ardhi na watu wenye ujuzi. Badala ya kutumia raslimali hizi, shule ziliwategemea wazazi maskini ili kupata pesa. Ikiwa shughuli za kuleta mapato zingeweza kuendelezwa shulenii, basi idadi ya watoto ambao walitoka ingepungua. Shule pia ziliangaliwa kama vituo ambapo ujuzi juu ya shughuli za kuleta mapato ungesambazwa katika jumuiya zilizo jirani ili hatimaye ziweze kuanzisha shughuli kama hizo nyumbani na kuwasaidia watoto wao. Kuanzisha na kusimamia shughuli za kuleta mapato kungekuwa kwenye kushirikisha wahusika wengi iwezekanavyoili kuhakikisha kwamba zitafaulu. Washika dau wote katika kiwango cha jumuiya, hasa wakuu wa shule, walimu, wazazi, kamati za kusimamia shule na wanafunzi wangeshirikishwa katika awamu zote.

#### Kuwaondoa Watoto Kutoka Kwenye Aina Mbaya Zaidi za ajira ya Watoto

Mpango huu ulijaribu kutambua aina mbaya zaidi za ajira ya watoto katika kiwango cha wilaya. Kwa kushirikiana na washika dau, mahitaji mbalimbali ya watoto wafanyakazi yalitambuliwa na njia za kuwaondoa kutoka kazini zilibuniwa. Utoaji wa elimu rasmi na isiyo rasmi na mafunzo ya kazi imetambuliwa kuwa mikakati muhimu ya kuwasaidia watoto walioondolewa kutoka kazini. Kwa hali hii kamati za ajira ya watoto zimevitambua vyuo vya ufundi anuawai kama asasi muhimu ambapo watoto walioondolewa kutoka kazini wangepata mafunzo ya kazi. Kupitia shughuli za kuleta mapato watoto walioondolewa kutoka kazini wakiwa na umri wa kuhuduria shule, walirudishwa shulenii na kusaidiwa.

Kupitia jitihada hizi, ANPPCAN imeimarisha kamati za Wilaya za Ajira ya Watoto na Kamati za Kutoa Ushauri za Tarafa. Watoto 1,583 wamefaidika moja kwa moja kutokana na mapato ya shughuli za kuleta mapato.

Wamepata sare za shule, ada za mitihani, vitabu, kalamu, n.k. Watoto wengine 3,850 wamefaidika kutokana na miradi ya shule kama vile ujenzi.

Mpango huu pia umesaidia vyuo vya ufundi anuawai 9 katika wilaya 9 ili viweze kuanzisha shughuli za kuleta mapato. Lengo ni kuwasaidia watoto walioondolewa kutoka kazini ili wapate mafunzo ya kazi. Kufikia sasa, watoto 154 waliokuwa wametolewa kazini wamesaidiwa kuingia shulenii na wengine 10 wameingia katika mafunzo ya kazi mahsusii.

Kufanya vyema masomoni kwa watoto kunahusishwa na idadi kubwa zaidi ya watoto kuingia shulenii na kubakia huko hadi mwisho. Hali hii imetokana na jitihada za pamoja za jumuiya, kamati za Wilaya za Ajira ya Watoto na ANPPCAN.

### **11. Juhudi Za Shirika La Amwik Kuinua Ufahamu**

Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) na Shirika la Wanawake katika vyombo vya Habari Nchini Kenya (AMWIK) yalianzisha juhudi za kampeni za kuinua ufahamu na kuimarisha uelewa wa umma na waunda sera juu ya ajira ya watoto kwa ujumla na hasa aina mbaya zaidi za ajira ya watoto.

Jitihada zimefanywa na kikundi hiki kuishawishi serikali na watoaji huduma wengine na pia kuimarisha uwezo wa waandishi wa habari kushughulikia ajira ya watoto. Haya yamefanywa kupitia vyombo vya habari. Kulingana na taarifa zilizopo, mahojiano yamefanywa yakilenga mipango ya IPEC nchini Kenya na pia sekta za kazi. Jitihada hizi zimekuwa muhimu katika kufahamisha kwamba malipo ya papo hapo ndicho chanzo cha kushiriki kwa watoto katika uvunaji wa kahawa, miraa, ukahaba wa watoto na uchongaji.

Ukaguzi wa gafla ulikuwa muhimu sana katika kubainisha aina mbaya zaidi za ajira nchini Kenya, k.m. kutembelea mashamba ya kahawa.

Ilibainika kwamba watoto walikuwa wakivuna kahawa katika mazingira ya hatari. Ilibainisha pia kwamba watoto wengi walikuwa wakifaidika kutokama na mipango ya IPEC kwa sababu wengi wao amba walikuwa wametoka shuleni walisharudi.

Kuingilia kati kwa KBC na AMWIK kunaweza kufichua na kuchapisha visa vya ajira ya watoto nchini. Hatua hii inaweza kuathiri sera juu ya ajira ya watoto.

Wanachama wa Kamati Elekezi na wawakilishi wa mashirika wanaofanya kazi kuhusiana na masuala ya ajira ya watoto wamealikwa mara kwa mara kuzungumzia suala hili. Masuala yanayohusika ni kama vile utungaji sheria, hasa kwa kutilia maanani kwamba Kenya ilishaidhinisha Maagano ya 182. Nyingi kati ya shughuli hizi zimeelekezwa kwenye mashirika yanayomiliki vyombo vya habari.

Mchakato wa kuinua kiwango cha ufahamu pia utatoa fursa ya watelelezaji kujifunza. Ili shughuli za kuinua kiwango chao ufahamu zifanikiwe, zafaa ziwe za muda mrefu na thabiti.

## **12. Machapisho yanayofaa kuhusu Mapatano ya 182.**

### **Machapisho ya Kiserikali.**

- ❖ Wasiliana na idara za serikali zilizo na wajibu wa utekelezaji (haswa wizara ya Afya) na ulizia machapisho kuhusu suala hili.

### **Machapisho yasiyo ya Kiserikali.**

- ❖ Global March Against Child Labour-

“ ILO Convention 182 Ending the Worst Forms Of Child Labour: A Guide to Action”, Mai 2000

Huu ni mwongozo wa Mkataba wa 182 ulio na utaratibu wa kisheria na wajibu wa Metambezi ya Dunia.

**Kipepesi: 00 91 11 6236818**

**Barua pepe: [childhood@globalmarch.org](mailto:childhood@globalmarch.org)**  
**[www.globalmarch.org](http://www.globalmarch.org)**

- ❖ **Save The Children UK**  
“Small Hands, Big Business”, Juni 2000

**Kipepesi: 00 44 20 7708 2508**

**Barua pepe: [publications@scfuk.org.uk](mailto:publications@scfuk.org.uk)**  
**[www.savethechildren.org.uk](http://www.savethechildren.org.uk)**

- ❖ **Defence For Children International, Costa Rica-**

“Prevencion y Eliminacion de las formas de trabajo infantile: un reto para la democracia y el desarollo humano”, Agosti 2000

**Kipepesi: 00506 283 1219**

**Barua pepe: [dnicos@sol.racsa.co.cr](mailto:dnicos@sol.racsa.co.cr)**

- ❖ **Anti- Slavery International/ Minority Rights Group International/**

“ Guide ILO Monitoring Mechanisms For Protecion Of Minorities, forthcoming 2001”

Huu ni mwongozo wa taratibu za ILO za kulinda haki za wachche, uliotarajiwa kuchapishwa 2001.

**Kipepesi: 00 44 20 77 38 4110**

**Barua pepe: [antislavery@antislavery.org](mailto:antislavery@antislavery.org)**

### **Machapisho ya ILO na yale ya IPEC, ya waajiri na ya waajiriwa.**

- ❖ **IPEC**

Iko na machapisho kadhaa kuhusu ajira ya watoto. Yanapatikana kuitia:

**Kipepesi: 00 41 22 799 8771**

Barua pepe: [ipec@ilo.org](mailto:ipec@ilo.org)

❖ ILO Bureau for Workers' Activities-  
ACTRAV"

ACTRAV ni idara ya ILO ya shughuli za wafanyakazina huratibu shughuli za afisi zinazohusisha mashirika ya waajiriwa katika makao makuu na katika kazi za nje.

Itachapisha mwongozo wa Mkataba wa ILO wa 182 unaotarajiwa kutoka mwaka wa 2001.

kipepesi: 00 41 2 799 6570

Barua pepe: [actrav@ilo.org](mailto:actrav@ilo.org)

[www.ilo.org](http://www.ilo.org)

❖ World Confederation of Labour  
(WCL)-

"International campaign for the ratification and Application of ILO Convention 182 Educational Hand book", Mei 2000.

kipepesi: 00 32 2 230 8722

[www.cmt-wcl.org/pubs/](http://www.cmt-wcl.org/pubs/)

## 12. Anuani za Mashirika Yanayohusika.

### Vyama vya wafanyakazi vya kimataifa.

ICFTU- International Confederation of Free Trade Unions, Bruxelles  
kipepesi: 0032 2 201 5815  
Barua pepe: [internetpo@icftu.org](mailto:internetpo@icftu.org)  
[www.icftu.org](http://www.icftu.org)

ICTFU African Regional Organisation (AFRO), Kenya  
kipepesi: 00 65 222 380  
Barua pepe: [icftuafro@formnet](mailto:icftuafro@formnet)

ICTFU-International Confederation of Free Trade Unions, Bruxelles  
kipepesi: 00 32 2 201 5815  
Barua pepe: [internetpo@ictfu.org](mailto:internetpo@ictfu.org)  
[www.ictfu.org](http://www.ictfu.org)

ICTFU African Regional Organisation (AFRO), Kenya

kipepesi: oo 254 221 5072

Barua pepe: [gs@ictfu-apro.org](mailto:gs@ictfu-apro.org)

ICTFU Inter-American Regional Organisatoin of Workers (ORIT), Venezuela,

kipepesi: 00 58 258 3349

Barua pepe: [orit@ven.net](mailto:orit@ven.net)

World Confederatoin of Labour, Bruxelles

kipepesi: 00 32 2 230 8722

Barua pepe: [info@cmt-wcl.org](mailto:info@cmt-wcl.org)

[www.cmt-wcl.org](http://www.cmt-wcl.org)

### Mashirika ya Kimataifa Ya Kiserikali

International Labour Organisation- International Programme for the Elimination of Child Labour (IPEC), Geneva

Simu: 0041.22.799.6486

kipepesi: 0041.22.799..8771

Barua pepe: [ipec@ilo.org](mailto:ipec@ilo.org)

[www.ilo.org/child labour](http://www.ilo.org/child_labour)

IPEC Regional Office for Asia, Bangkok

kipepesi: 00 66 2 288 1069

Barua pepe: [manghas@ilo.org](mailto:manghas@ilo.org)/[rahman@ilo.org](mailto:rahman@ilo.org)

IPEC Sub rergional Office fo Central America, San Jose

kipepesi: 00 506 280 6991

Barua pepe: [ipec@oit.or.cr](mailto:ipec@oit.or.cr)

IPEC Sub- Regional Office for South America, Lima

kipepesi: 00 51 1 421 5292

Barua pepe: [cuadro@ilo.org](mailto:cuadro@ilo.org)

IPEC Regional Office for Francophone Africa, Abidjan

kipepesi: 00 255 212880,

Barua pepe : [d'ovidio@ilo.org](mailto:d'ovidio@ilo.org) ama [roeske@ilo.org](mailto:roeske@ilo.org)

IPEC Area Office for Anglophone Africa, Dar es Salaam,

kipepesi: 00255 52 666004

Barua pepe: [singhs@ilo.org](mailto:singhs@ilo.org)

Ofisi kuu Ya UNICEF, New York,

kipesepi: oo 1 212 887 7465

[www.unicef.org](http://www.unicef.org)

## Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali

International Save the Children Alliance

kipesepi: 00 44 20 8237 8000

Barua pepe: [info@save-children-alliance.org](mailto:info@save-children-alliance.org)  
[www.savethechildren.net](http://www.savethechildren.net)

International Federation Terre des Hommes

kipesepi: 00 41 22 736 15 10

Barua pepe: [intl-rel@iftdh.org](mailto:intl-rel@iftdh.org)  
[www.iftdh.org](http://www.iftdh.org)

Defence For Children International

kipesepi: 00 41 22 740 1145

Barua pepe: [dci-hq@pingnet.ch](mailto:dci-hq@pingnet.ch)  
[www.defence.for-children.org](http://www.defence.for-children.org)

World Vision International

kipesepi: 00 41 22 798 6547

Barua pepe: [geneva@wvi.org](mailto:geneva@wvi.org)  
[www.wvi.org](http://www.wvi.org)

Anti-Slavery International

kipesepi: 00 44 20 7738 4110

Barua pepe: [info@antislavery.org](mailto:info@antislavery.org)  
[www.antislavery.org](http://www.antislavery.org)

Coalition to stop the Use of Child Soldiers

S.L.P. 22696, London, N4 3ZJ, UK.

Barua pepe: [info@childsoldiers.org](mailto:info@childsoldiers.org)

[www.child-soldiers.org](http://www.child-soldiers.org)

International Service for Human Rights

kipesepi: 00 41 22 733 0826

[www.ishr.ch](http://www.ishr.ch)

Child Workers in Asia,

kipesepi: 00 662 215 8272

Barua pepe: [cwanet@oxinfo.co.th](mailto:cwanet@oxinfo.co.th)

ECPAT International (End Child Prostitution, Pornography and the Trafficking of Children for Sexual Purposes)

kipesepi: 00 662 215 8572

Barua pepe: [eccpatbkk@ksc15.th.com](mailto:eccpatbkk@ksc15.th.com)  
[www.eccpat.net](http://www.eccpat.net)

ANPPCAN (African Network for the Prevention and Protection Against Child Abuse and Neglect)

kipesepi: 00254 2 57 65 02

Barua pepe: [anppcan@arcc.or.ke](mailto:anppcan@arcc.or.ke)

[www.africaonline.do.ke/anppcan/](http://www.africaonline.do.ke/anppcan/)

Consortium For Street Children

kipesepi: 00 44 20 7738 4110

Barua pepe: [cscuk@gn.apc.org](mailto:cscuk@gn.apc.org)  
[www.csuk.org.uk](http://www.csuk.org.uk)

Mashirika ya Kimataifa Ya Waajiri.

ILO Bureau For Employers' Activities

(ACT/EMP)

Simu: 00 41 22 799 7748

kipesepi: 00 41 22 799 8948

Barua pepe: [actemp@ilo.org](mailto:actemp@ilo.org)

(Orodha ya anwani na anwani za mitandao ya Mashirika rasmi ya Waajiri ulimwenguni kote yanaweza kupatikana katika: <http://www.ilo.org/public/english/dialogue/actemp/contact/emp-org.htm>)

**International Organisation for Employers (IOE),**

Simu : 00 41 22 798 16 16

kipesepi: 00 41 22 798 88 62

Barua Pepe: [ioe@ioe-emp.org](mailto:ioe@ioe-emp.org)

**Miungano ya Kitaifa ya Haki za Watoto**

Miungano hii inaweza kufikiwa kupitia

Mtandao Wa Maelezo Kuhusu Haki Za Watoto (Child Rights Information Network) kupitia anwani ya mtandao [www.Crin.org](http://www.Crin.org).

Kwa vingine, maelezo mengine yanaweza kupatikana kupita Kundi la Mashirika yasiyo ya Serikali la Geneva, sehemu ya Mawasiliano kupitia kwa :

Defence For Children International,

kipesepi: 0041 22 1145

Barua pepe: [dci-ngo.group@pingnet.ch](mailto:dci-ngo.group@pingnet.ch).

**Mashirika ya Kimataifa ya Watoto wanaofanya kazi.**

ENDA Jeunesse Action

African Movement of Child and Youth Workers

kipesepi: 00 221 823 51 57

Barua pepe: [jeuda@enda.sn](mailto:jeuda@enda.sn)  
[www.enda.sn/eja](http://www.enda.sn/eja)

**NATs Ninos/as y Adolescentes Trabajadores**  
**Latin American Working children's**  
**coordinationg organisaton**  
**kipepesi: 00 511 466 4789,**  
**Barua pepe: mnatsop@perudata.com**

**Concern for Working Children/Bhima Sangha**  
**South Asian working children's Organisation**  
**kipepesi: 00 91 80 523 4258**  
**Barua pepe: cwc@pobox.com**  
**www.workingchild.org**

### **Kundi la Mashirika Yasiyo Ya**

### **Kiserikali la CRC**

**Iina ofisi iliyomo –Geneva:**  
**kupita kwa :**  
“Defence For Children International”,  
S.L.P. 88,  
1211 GENEVA 20,  
Switzerland.

**Kipepesi: 00 41 22 740 1145**  
**Barua pepe: ngo.group@pingnet.ch.**

### **Kikundi kidogo cha Ajira ya**

### **Watoto:**

**Kina makao katika ‘Anti-slavery**  
**Interantional’:**

**Thomas Clarkson Hse.**  
**The Stableyard,**  
**Broomgrove Road,**  
**London SW9 9TL,**  
**U.K.**

**kipepesi: 00 44 20 7738 4110**  
**Barua pepe: antislavery@antislavery.org**  
**www.antislavery.org**

**Do you know...**

**about the new ILO Worst Forms of Child Labour Convention?**